



# Sauti za Waandishi

## Utafiti wa Sauti za Waandishi wa Habari Tanzania.

## 1. Utangulizi

Waandishi wa habari wana nafasi muhimu sana katika jamii. Vyombo vya habari huwapatia wananchi taarifa kuhusu maendeleo na matukio mbalimbali yanayotokea kila siku. Vyombo vya habari pia vinafanya kazi ya kuwawajibisha wenye madaraka na vinatoa nafasi kwa mijadala ya kitaifa kufanyika. Vile vile vyombo hivi ni jukwaa huru kwa wananchi kupaza sauti zao. Kutokana na umuhimu huo, ni vema kufahamu uzoefu na maoni ya waandishi wa habari ambao ni nguzo muhimu ya mustakabali wa maendeleo ya jamii.

Je, waandishi wa habari wana hali gani ya ajira? Je, wanapata kipato cha kutosha? Na je, wanaridhika na kazi zao? Mara ngapi wanakumbana na vitisho na unyanyasaji kutokana na kazi zao, na vitisho hutoka kwa nani? Wana mtazamo gani kuhusu uhuru wa vyombo vya habari kwa nadharia na kwa vitendo? Na wana matarajio gani ya mustakabali wa taaluma yao nchini?

Muhtasari huu unawasilisha takwimu kuhusu uzoefu na maoni ya waandishi wa habari wa Tanzania. Maoni haya yalikusanywa kutoka kwa waandishi wa habari, wahariri na wanablogu 1,202. Jopo hilo liliundwa kutokana na kanzidata za uanachama wa vyama mbalimbali vya habari ambavyo ni Chama cha Vilabu vya Waandishi wa Habari Tanzania (UTPC), Chama cha Wanawake Waandishi wa Habari Tanzania (TAMWA), Taasisi ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika Tawi la Tanzania (MISA-Tan) na Jamii Forums. Mahojiano yalifanywa kwa njia ya simu kati ya Septemba 23 na Novemba 7, 2023.

Ikizingatiwa kwamba waandishi wengi wa habari nchini ni wanachama wa vilabu vya

Muhtasari huu umeandikwa na umeandaliwa na Twaweza East Africa.

S.L.P 38342, Dar es Salaam, Tanzania. +255 22 266 4301 | info@twaweza.org | www.twaweza.org/sauti

Sauti za Wananchi

waandishi wa habari vya kikanda (pamoja na UTPC), utafiti huu unaweza kuwa na sura ya kitaifa kwa maana una uwakilishi wa kiasi kikubwa wa uzoefu na maoni wa waandishi wa habari nchini Tanzania.

Matokeo Muhimu ya utafiti huu ni kama ifuatavyo:


- Waandishi wengi wa habari wana aina za ajira zisizo za kudumu na zisizotegemewa
- Waandishi wa habari wengi wanasema ni vigumu kupata kipato kinachokidhi mahitaji yao kutokana na kazi yao ya uandishi
- Waandishi wengi wa habari wameridhika na kazi yao ya sasa, ingawa wengi wasingependa watoto wao kuwa waandishi wa habari
- Wanahabari wanawake wanahisi kwamba hawatendewi haki mara zote ikilinganishwa na wanahabari wenzao wanaume.
- Nusu ya waandishi wa habari wameripoti kwamba wamewahi kutishiwa, kunyanyaswa au kushambuliwa kipindi fulani
- Waandishi wa habari wanawanyooshea kidole maafisa wa serikali kama chanzo kikuu cha vitisho kwa kazi yao
- Waandishi wa habari wanasema huwa wanahakiki ukweli katika ripoti zao, lakini wengi wako tayari kulegeza msimamo pale inapowalazimu kufanya hivyo
- Waandishi wa habari wanatambua sana uwepo wa rushwa ndani ya vyombo vya habari
- Waandishi wa habari wanakubali kimsingi kwamba vyombo vya habari vinapaswa kuwa huru na visiingiliwe na serikali, lakini wanakubali mipaka katika maeneo maalumu
- Waandishi wengi wa habari wanahisi kwamba vyombo vya habari nchini Tanzania havina uhuru wa kutosha wa kufanya kazi zao
- Waandishi wa habari wanasema kuna taarifa ambazo haziwezi kuripotiwa
- Waandishi wa habari wanaona changamoto za kiuchumi kama kikwazo kikubwa kwenye uhuru wa vyombo vya habari
- Waandishi wa habari nchini Tanzania wanatarajia mabadiliko mengi na changamoto katika miaka 5-10 ijayo, lakini wana matumaini makubwa
- Waandishi wengi wa habari wanatarajia nafasi ya waandishi wa habari kubadilika, lakini si kutoweka

# 2. Mambo 15 kuhusu Uzoefu na Maoni ya Waandishi wa Habari Tanzania.

## Jambo la 1. Jopo linawakilisha sehemu pana ya waandishi wa habari

Jopo lina wanaume wengi zaidi (56%) kuliko wanawake (44%), jambo ambalo linaakisi hali halisi ya idadi ya wanaume na wanawake walioajiriwa katika sekta hii. Wachache wana umri wa miaka 25 au chini (4%), karibia nusu (45%) wana miaka 35 au chini. Wanachama wengi wa jopo wana zaidi ya elimu ya sekondari; kama vile stashahada (63%), shahada ya uzamili au zaidi (22%) au cheti (11%). Wanachama wa jopo wako katika mikoa yote iliyopo nchini, yaani bara na visiwani.


**Kielelezo cha 1: Muundo wa jopo la Sauti za Waandishi, ikiwa ni pamoja na eneo la kijiografia:**




**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Waandishi,* Septemba - Novemba 2023
Msingi: wahojiwa wote (n=1,202)

Wanachama wa jopo wanajumuisha aina zote za vyombo vya habari, ikiwa ni pamoja na vyombo vya habari vya mtandaoni na visivyo vya mtandaoni (online/offline). Redio (43%) inaongoza, ikifuatiwa na magazeti (25%), televisheni (23%), televisheni ya mtandaoni (6%), na blogu (5%). Aidha, wanawakilisha sehemu mbalimbali za vyombo vya habari vya binafsi na vya serikali, ingawa vyombo vya habari vya binafsi vinaongoza (72%).

**Kielelezo cha 2: Unafanya kazi katika aina gani ya chombo cha habari?** *(majibu mengi)*
**Nani anamiliki chombo kikuu cha habari unachofanyia kazi?** *(jibu moja)*





**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Waandishi,* Septemba - Novemba 2023
Msingi: wahojiwa wote (n=1,202)

## Jambo la 2. Waandishi wengi wana ajira zisizo za kudumu na zisizotegemewa

Wawili kati ya kumi (20%) wanataja hali yao ya ajira kama ya kudumu, ikilinganishwa na sita kati ya kumi (60%) wanaosema ni ya muda mfupi na wawili kati ya kumi (18%) wanaosema ajira yao ni pale wanapohitajika tu. Nusu (50%) wana mkataba uliosainiwa.

**Kielelezo cha 3: Katika chombo chako kikuu cha habari, je, unaelezeaje vigezo vya ajira yako? Je, kuna mkataba / makubaliano yaliyosainiwa?**





**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Waandishi,* Septemba - Novemba 2023
Msingi: wahojiwa wote (n=1,202)

Waandishi wengi wa habari hawapokei mafao ya ajira kama pensheni, bima na likizo za malipo. Nusu (50%) wana aina fulani ya bima ya afya, wanne kati ya kumi (38%) wana mpango wa pensheni na watatu kati ya kumi (28%) wamesajiliwa kulipa kodi ya mapato. Chini ya wawili kati ya kumi wanapokea likizo ya mwaka yenye malipo (16%) au likizo ya uzazi (15%).

Masharti haya ya kazi ni sawa kwa wanaume na wanawake, isipokuwa kwa likizo ya uzazi yenye malipo, ambapo waandishi wa habari wanawake wana uwezekano mkubwa zaidi kupata likizo hii kuliko wanaume, ingawa idadi bado ni wawili kati ya kumi (20%) miongoni mwa wanawake. Hata hivyo, wale wenye ajira ya kudumu wana manufaa bora zaidi yanayotokana na ajira.

**Kielelezo cha 4: Je, una yoyote kati ya yafuatayo?**





**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Waandishi,* Septemba - Novemba 2023
Msingi: Wahojiwa wote (n=1,202)

## Jambo la 3. Waandishi wa habari wengi wanasema ni vigumu kupata kipato kinachokidhi mahitaji yao kutokana na kazi yao ya uandishi

Waandishi wa habari wengi (63%) wanasema ni vigumu kupata kipato kinchokidhi mahitaji kutokana na uandishi wa habari, huku wachache sana (5%) wakisema ni rahisi. Mmoja kati ya waandishi watatu (36%) hufanya kazi nyingine yenye malipo mbali na kazi ya uandishi wa habari – hasa ujasiriamali na biashara (22% haijaoneshwa kwenye kielelezo).

**Kielelezo cha 5: Ni rahisi au vigumu kiasi gani kupata kipato kipato kinachokidhi mahitaji kutokana na uandishi wa habari? Mbali na kufanya kazi katika vyombo vya habari, je, una kazi nyingine zenye malipo?**





**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Waandishi,* Septemba - Novemba 2023
Msingi: wahojiwa wote (n=1,202)

## Jambo la 4. Waandishi wa habari wengi wameridhika na kazi yao ya sasa, lakini wengi wasingependa watoto wao (wa kiume au wa kike) waje kuwa waandishi wa habari.

Nusu ya waandishi wa habari (53%) wanasema wameridhika kabisa na kazi yao, sita kati ya kumi (58%) wana motisha kubwa ya kufanya kazi katika sekta hiyo, na nusu (53%) wangechagua tena uandishi wa habari. Hata hivyo, mmoja kati ya watatu anafikiria kuacha kazi ya uandishi wa habari (35%) na wawili tu kati ya kumi (19%) wangependa watoto wao wawe waandishi wa habari.

**Kielelezo cha 6: Je, unakubaliana au unapingana na kauli zifuatazo?**





**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Waandishi,* Septemba - Novemba 2023
Msingi: wahojiwa wote (n=1,202)

Waandishi wengi wanasema walichagua kazi hii kwa sababu ya thamani inayoleta kwa jamii (61%) kuliko walioichagua kwa sababu ni kazi nzuri (39%). (Haijaonyeshwa katika kielelezo).

## Jambo la 5. Wanahabari wanawake wanahisi kwamba hawatendewi haki mara zote ikilinganishwa na wenzao wanaume.

Wanahabari wengi wanawake wanahisi kwamba hawatendewi haki mara kwa mara ikilinganishwa na wanahabari wanaume, hasa katika masuala yanayohusu fedha na kupandishwa vyeo. Wanahisi kwamba wanatendewa kwa haki zaidi linapokuja suala la kupata fursa za kuripoti habari fulani au kuchapisha au kutangaza kazi zao.


**Kielelezo 7: Ukiwa kama mwandishi wa habari wa kike, unazungumziaje mahusiano yako na viongozi wa juu ukilinganisha na mahusiano yao na waandishi wa kiume?**




**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Waandishi,* Septemba - Novemba 2023
Msingi: wahojiwa wa kike (n=527)

Wanahabari wa kike na wa kiume wanaripoti mada tofauti: wanawake wengi zaidi kuliko wanaume wanapangiwa kuripoti kuhusu masuala ya jinsia na afya, wanaume wanaripoti zaidi kuhusu siasa na michezo.

**Kielelezo cha 8: Ni eneo gani kuu la mada unaloripoti zaidi?** *(Jibu moja)*





**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Waandishi,* Septemba - Novemba 2023
Msingi: wahojiwa wote (n=1,202)

## Jambo la 6. Nusu ya waandishi wa habari wameripoti kwamba wamewahi kutishiwa, kunyanyaswa, au kushambuliwa kipindi fulani.

Uzoefu wa waandishi wa habari kuhusu usalama wa kazi yao ni mkubwa. Nusu (50%) wameripoti kwamba wamewahi kutishiwa, kunyanyaswa, au kushambuliwa kipindi fulani, ikiwa ni pamoja na mmoja kati ya kumi (11%) ambao wamekumbana na hili katika miezi kumi na mbili iliyopita.

Wawili kati ya kumi (22%) wamekamatwa au kushikiliwa na mamlaka, na idadi inayofanana na hiyo wamekumbana na unyanyasaji wa kingono (20%) au vifaa au nyaraka zao kuchukuliwa (20%). Idadi kubwa (14%) wamekumbana na vitisho dhidi ya rafiki au mwanafamilia.


**Kielelezo cha 9: Ukiwa kama mwandishi wa habari, je, umewahi kukumbana na yafuatayo mwaka uliopita au kipindi fulani?**




**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Waandishi,* Septemba - Novemba 2023
Msingi: wahojiwa wote (n=1,202)

Waandishi wa habari wa kiume wanaripoti kupitia unyanyasaji, vitisho, n.k., zaidi ya waandishi wa habari wa kike. (Hii inaweza kuwa imeunganishwa na maeneo tofauti wanayoripoti – angalia Kielelezo namba 9 hapo juu). Wale walio katika ajira ya kudumu wanaripoti kupitia matatizo haya mara chache zaidi kuliko wale walio katika aina za ajira za muda mfupi au za kipindi maalumu.

**Kielelezo cha 10: Je, umewahi kukumbana na yafuatayo katika kazi yako kama mwandishi wa habari?**





**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Waandishi,* Septemba - Novemba 2023
Msingi: wahojiwa wote (n=1,202)

## Jambo la 7. Waandishi wa habari wanawatuhumu maafisa wa serikali kama chanzo kikuu cha vitisho katika kazi zao.

Waandishi wa habari kwa kiasi kikubwa wanawatuhumu maafisa wa serikali kama chanzo kikuu cha vitisho kwa kazi zao. Zaidi ya nusu (56%) wanasema maafisa wa serikali ni chanzo kikuu cha vitisho, zaidi ya kikundi kingine chochote. Hii inafuatiwa na polisi na wakala wengine wa usalama (13%) na wasimamizi wa kazi zao (8%). Wawili kati ya kumi (20%) wanaripoti hawajakabiliwa na vitisho vyovyote.

**Kielelezo cha 11: Kwa ujumla, ni nini au nani chanzo kikubwa cha vitisho kwa kazi yako?**





**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Waandishi,* Septemba - Novemba 2023
Msingi: wahojiwa wote (n=1,202)

Waandishi wengi wa habari (87%) wanasema waajiri wao hawatoi ulinzi wa maana kwa usalama wao. (Haijaoneshwa kwenye kielelezo).

## Jambo la 8. Waandishi wa habari wanasema wako makini kuhakiki ukweli katika kuripoti kwao, lakini wengi wako tayari kulegeza msimamo pale inapowalazimu kufanya hivyo.

Waandishi wa habari wanasema wako makini kuhakiki ukweli kabla ya kuripoti kwao, ambapo tisa kati ya kumi (92%) wanasema wanafanya hivyo; lakini wengi wako tayari kulegeza msimamo katika baadhi ya maeneo pale wanapolazimika kufanya hivyo. Nusu (52%) wanasema kuwa wakati mwingine mbinu zenye utata zinakubalika ili kupata habari muhimu kwa umma, na watatu kati ya kumi (28%) wanasema wakati mwingine ni lazima kuripoti mambo chanya kuhusu watu wenye nguvu ili kubaki salama.

**Kielelezo cha 12: Je, unakubaliana au unapingana na kauli zifuatazo?**





**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Waandishi*, Septemba - Novemba 2023
Msingi: wahojiwa wote (n=1,202)

## Jambo la 9. Waandishi wa habari wanatambua uwepo wa rushwa ndani ya vyombo vya habari.

Karibia waandishi wote wa habari (86%) wanasema rushwa ipo katika sekta hiyo, ikiwa ni pamoja na (36%) wanaosema kwamba imeenea sana. Aina za kawaida za rushwa ni malipo kwa ajili ya kuchapisha (55%) au kutokuchapisha (53%) habari fulani.

**Kielelezo cha 13: Je, kuna rushwa kwa kiwango gani katika vyombo vya habari Tanzania? Eleza aina ya rushwa/utendaji mbaya:**





**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Waandishi,* Septemba - Novemba 2023
Msingi: wahojiwa wote (n=1,202)

Karibu wote (95%) wanasema hupokea pesa kutoka kwa watu au taasisi zinazohusika na habari husika. Hiyo hutokea kila mara (23%) au mara kadhaa (72%). Idadi inayofanana na hiyo inasema waandishi wa habari hupokea zawadi, safari za bure, n.k.

Zaidi ya nusu (76%) wanasema waandishi wa habari wakati mwingine huomba motisha ili kufunika au kuepuka habari fulani na idadi inayofanana na hiyo inaripoti kuwa wamepewa motisha ili kufunika au kuepuka habari.

Mmoja kati ya kumi (10%) anaripoti kuwa "mara nyingi" amepokea zawadi na pesa ili kushawishi maudhui, na nusu nyingine (53%) wanasema wamefanya hivyo mara kadhaa.

**Kielelezo cha 14: Je, ni mara ngapi yafuatayo hutokea Tanzania?**





**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Waandishi,* Septemba - Novemba 2023
Msingi: Wahojiwa wote (n=1,202)

## Jambo la 10. Waandishi wa habari wanakubaliana na kanuni kwamba vyombo vya habari vinapaswa kuwa huru bila kudhibitiwa na serikali, lakini wanakubali mipaka katika maeneo maalumu.

Waandishi wa habari wanakubaliana sana na kanuni kwamba vyombo vya habari vinapaswa kufanya kazi kwa uhuru mkubwa bila kudhibitiwa na serikali. Idadi kubwa (86%) wanapendelea kauli kwamba vyombo vya habari vinapaswa kuwa na haki ya kuchapisha chochote bila udhibiti wa serikali, wakati wachache (14%) wanapendelea kauli mbadala: kwamba serikali inapaswa kuwa na haki ya kuzuia vyombo vya habari kuchapisha mambo ambayo inayakataa.

Vivyo hivyo, idadi kubwa wanapendelea mtazamo kwamba kama chombo cha habari kitachapisha au kutoa taarifa isiyo sahihi kiombe radhi na kuchapisha taarifa sahihi. Na wengi wanaona kuripoti makosa ya serikali na rushwa kama kitu chanya, badala ya kitu kinachodhoofisha nchi.

**Kielelezo cha 15. Kutoka kila fungu la kauli, ni ipi unakubaliana nayo zaidi?**





**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Waandishi,* Septemba - Novemba 2023
Msingi: wahojiwa wote (n=1,202)

Hata hivyo, waandishi wa habari wana hisia mchanganyiko kuhusu Serikali kuzuia habari au taarifa zisizo za kweli, zinazokosoa au zilizo hasi. Kwa mfano, sita kati ya kumi (60%) wanakubaliana kwamba serikali inapaswa kuwa na uwezo wa kuzuia habari au taarifa ambazo si sahihi na hazina ukweli.

Vivyo hivyo, wanne kati ya kumi (42%) wanasema ni sahihi kwa serikali kuzuia ukosoaji au matusi yanayoelekezwa kwa Rais, na watatu kati ya kumi (32%) wanasema ni sahihi kwa serikali kuzuia uchapishaji wa habari zinazoishushia hadhi serikali. Ni katika kizuizi hiki cha mwisho cha serikali ambacho waandishi wa habari wengi wanaona kama hakina msingi.

**Kielelezo cha 16: Je, unakubaliana au haukubaliani kwamba serikali inapaswa kuwa na uwezo wa kuzuia au kupiga marufuku kusambaza habari au taarifa ambayo ...?**





**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Waandishi,* Septemba - Novemba 2023
Msingi: wahojiwa wote (n=1,202)

## Jambo la 11. Waandishi wa habari wengi wanahisi kwamba vyombo vya habari nchini Tanzania havina uhuru wa kutosha wa kufanya kazi zao.

Waandishi wa habari wengi (62-68%) wanasema kwamba vyombo vya habari haviko huru kuripoti na kutoa maoni kuhusu habari bila kudhibitiwa au kuingiliwa na wamiliki wa vyombo hivyo, serikali, watu wenye mamlaka na makampuni binafsi.

Vivyo hivyo, wengi wanasema hawajisikii huru kukosoa kauli na maamuzi ya serikali bila hofu, na idadi kubwa (40%) wanasema vyombo vya habari vinajidhibiti ili kulinda wanahabari wake au maslahi yake.

**Kielelezo cha 17: Je, unakubaliana au hukubaliani na kauli hizi?**





**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Waandishi,* Septemba - Novemba 2023
Msingi: wahojiwa wote (n=1,202)

## Jambo la 12. Waandishi wa habari wanasema kuna mada ambazo haziwezi kuripotiwa

Wakati wanahabari wanahisi wako huru kwa kiasi kikubwa kuripoti kuhusu masuala ya kidini na kiuchumi, hali ni tofauti kwenye masuala ya haki, rushwa, na vyombo vya ulinzi na usalama. Wanahabari sita kati ya kumi wanasema hawajisikii huru kabisa kuripoti kuhusu rushwa (60%) au masuala yanayohusiana na vyombo vya ulinzi na usalama (61%).


**Kielelezo cha 18: Kama mwandishi wa habari, unajisikia huru kwa kiasi gani kuripoti kuhusu yafuatayo?**




**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Waandishi,* Septemba - Novemba 2023
Msingi: wahojiwa wote (n=1,202)

Waandishi wa habari pia hawajisikii huru kufuatilia habari nyeti zinazoigusa serikali au watu wenye mamlaka. Waandishi wa habari wachache wanasema wako huru kufuatilia habari zenye maslahi ya umma, kupata rekodi za serikali, kufuatilia habari zinazohusiana na rushwa, kufichua makosa ya serikali na kukosoa na kuchambua kauli na matendo ya serikali.

**Kielelezo cha 19: Kama mwandishi wa habari, uko huru kufanya yafuatayo?**





**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Waandishi,* Septemba - Novemba 2023
Msingi: wahojiwa wote (n=1,202)

## Jambo la 13. Waandishi wa habari wanaona changamoto za kiuchumi kama kikwazo kikubwa kwenye uhuru wa vyombo vya habari.

Wanahabari saba kati ya kumi (68%) wanakubaliana kwamba leseni na ada za usajili ni ghali. Nusu (52%) wanasema kwamba vyombo vya habari wakati mwingine vinalazimika kubadilisha maudhui yao ili kupata matangazo ya serikali.

**Kielelezo cha 20: Je, unakubaliana kwa kiasi gani au hukubaliani na kauli zifuatazo?**




**Chanzo cha Takwimu**: Utafiti wa *Sauti za Waandishi,* Septemba - Novemba 2023
Msingi: wahojiwa wote (n=1,202)


## Jambo la 14. Waandishi wa habari nchini Tanzania wanatarajia mabadiliko mengi katika kipindi cha miaka 5 -10 ijayo, lakini wana matumaini makubwa

Waandishi wa habari nchini Tanzania wanatarajia mabadiliko mengi katika kipindi cha miaka 5 -10 ijayo, lakini wana matumaini makubwa kuhusu mustakabali wa sekta yao. Wengi wanakubaliana au wanakubaliana sana kwamba uandishi wa habari utahusisha kazi zaidi na wataalamu wa teknolojia (84%), kwamba waandishi wa habari watahitaji kupata ujuzi mpya (80%), na kwamba majukwaa ya mtandaoni na kidijiti yatatawala (74%).

Wengi wanakubali au wanakubali sana kwamba mitandao ya kijamii imepunguza uaminifu wa tasnia ya uandishi wa habari (73%), na kwamba mfano uandishi wa habari wa magazeti na matangazo hivi karibuni utakuwa haufai tena (65%).

Hata hivyo, wengi (60%) pia wanakubaliana kwamba tasnia ya vyombo vya habari itakuwa inastawi katika miaka 5 - 10 ijayo.

**Kielelezo cha 21: Unakubaliana kwa kiasi gani au hukubaliani na kauli zifuatazo?**





**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Waandishi,* Septemba - Novemba 2023
Msingi: wahojiwa wote (n=1,202)

## Jambo la 15. Waandishi wa habari wengi wanatarajia nafasi ya waandishi wa habari kubadilika, lakini sio kutoweka

Waandishi wa habari wengi (75%) wanategemea nafasi ya waandishi wa habari kubadilika katika miaka 5 -10 ijayo, au kwamba itapanuka (17%). Wachache (6%) wanafikiri itapungua au kutoweka, na wachache zaidi (1%) wanategemea itabaki bila mabadiliko.

**Kielelezo cha 22: Unadhani nafasi ya waandishi wa habari itabadilikaje katika kipindi cha miaka 5-10 ijayo?**




**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Waandishi,* Septemba - Novemba 2023
Msingi: wahojiwa wote (n=1,202)

## 3. Hitimisho

Muhtasari huu unawasilisha matokeo ya utafiti wa kipekee nchini Tanzania uliokusanya uzoefu na maoni ya waandishi wa habari kuhusu masuala mbalimbali yanayohusiana na taaluma yao. Pamoja na yote, matokeo makuu manne yanajitokeza.

Kwanza, ni dhahiri kwamba uandishi wa habari – na sekta ya vyombo vya habari kwa ujumla – inakabiliwa na vikwazo vikubwa vya kifedha. Waandishi wa habari wengi wanasema kwamba ni vigumu kupata riziki kutokana na uandishi wa habari. Na wanataja mambo mengi ikiwemo mifumo migumu ya kibiashara kwa wamiliki binafsi wa vyombo vya habari, kupunguza uhuru wa vyombo vya habari hasa kuripoti kuhusu taasisi fulani au mada fulani. Na ingawa waandishi wa habari wengi wameridhika na chaguo lao la kazi, wasingependa watoto wao kufuata nyayo zao. Kwa maana nyingine, waandishi wa habari wanaona uandishi wa habari kama kazi yenye maana, lakini si bora; ni kazi ya mtu ambaye anaweza kuona fursa zilizopo lakini si ya mtu mwenye malengo na ndoto za kutajirika.

Pili, waandishi wa habari wanakiri kwamba rushwa na vitendo visivyo vya kimaadili vimeenea ndani ya vyombo vya habari. Kwa namna fulani, hili linahusiana na hoja ya kwanza: ikiwa njia pekee ambayo mwandishi wa habari anaweza kumudu kuandika habari ni kukubali nauli au hata pesa kutoka kwa waandaaji, si rahisi kuepuka uwasilishwaji wao kimaudhui kuathiriwa. Mwanahabari anayepambana kufanya kazi kwa bidii kugharamia mahitaji yake ya msingi atakuwa hatarini zaidi kushawishiwa na watu mwenye mamlaka, wakiwemo wahariri na wamiliki wa vyombo vya habari, ili aandike habari “nzuri” au kuacha habari “mbaya.”

Tatu, waandishi wa habari wanavyo vikwazo vingine vya uhuru wao mbali na masuala ya kiuchumi. Wanaelezea vikwazo vya ufanisi wa kazi zao kutoka kwa wamiliki wa vyombo vya habari, serikali na watu wenye mamlaka, na kuona kwamba baadhi ya mada haziruhusiwi kuripotiwa. Ingawa waandishi wa habari wako wazi kwamba kimsingi, vyombo vya habari vinapaswa kuwa huru kufanya kazi bila kudhibitiwa na serikali, linapokuja suala la kutoa mifano halisi, kauli yao inabadilika kidogo. Wachache wanakubali serikali kuzuia uchapishaji wa chochote kinachoharibu taswira ya serikali.

Mwisho, wanahabari wengi wanakumbana na vitisho wakiwa kazini. Nusu wametishiwa, kunyanyaswa au kushambuliwa katika kipindi fulani. Idadi kubwa wamekamatwa au kuzuiliwa, kupata unyanyasaji wa kijinsia au kunyang'anywa vitendeakazi vyao. Wanabainisha kuwa mamlaka za serikali ndio chanzo kikuu cha vitisho. Wanaripoti kwamba waajiri wao hutoa ulinzi mdogo sana dhidi ya hatari wanazokabiliana nazo. Lakini ni vyema kutambua kwamba wale wenye mikataba ya ajira ya kudumu wanaonekana kuepuka vitisho na unyanyasaji kwa kiasi kikubwa zaidi.

Picha kuu inayotokana na utafiti huu ni kwamba kazi za uandishi wa habari nchini Tanzania ni ngumu sana. Wanahabari wanaitambua thamani ya kazi yao, lakini wanapitia changamoto nyingi – kiuchumi, kiusalama, kisiasa, kisheria, kijamii – zinazowakwamisha. Changamoto hizi zikipungua au kuondoka kabisa, wanahabari wataweza kutekeleza vyema majukumu yao muhimu ndani ya jamii, yakiwemo kuwahabarisha, kuwaelimisha na kuwaburudisha wananchi, pamoja na kuwawajibisha wenye mamlaka.

Kuna uhitaji mkubwa wa kutengeneza mazingira itakayowaruhusu waandishi wa habari kufanya kazi kwa uhuru zaidi na kuchangia maendeleo ya taifa. Wanahabari wanayo haki ya kulindwa dhidi ya vitisho na unyanyasaji. Wanastahili kuwa na mikataba ya kazi na yenye maslahi mazuri. Sheria ziwalinde wanahabari, na siyo kuwatisha ili ukweli usiibuke. Nafasi ya waandishi wa habari katika jamii ni muhimu; sisi sote tunapaswa kufanya kila tuwezalo kuwalinda na kuwastawisha.